JUMANNE

Niliamshwa majira ya saa kumi na moja za asubuhi kwa mlio wa ndege walioanza kuimba kwa kupokezana wakisindikizwa na sauti ya upepo uliokuwa ukivuma taratibu. Kwa mbali niliweza kuanza kusikia majogoo ya mwanzo yakiisalimu siku kwa kupokezana. Nilifumbua macho yangu na kuyapepesa kwa sekunde kadhaa kuweza kuanza kuupokea mwanga hafifu wa siku mpya uliokuwa unatangulia jua kuchomoza. Mme wangu Waziri alikuwa amelala pembeni yangu. Sikumbuki aliingia nyumbani saa ngapi jana usiku kwani mida aliyofika nilikuwa nimeshauchapa usingizi. Nilienda kulala mapema kidogo baada ya kuteremshia chakula cha jioni na bia mbili za Safari. Kwa kawaida huwa nafanya kazi kidogo hadi karibu saa sita za usiku lakini siku hiyo nilikuwa nimechoka kweli.

Nilimuangalia mume wangu ambaye bado alikuwa katika usingizi fofofo. Nilitamani nimguse nimuamshe nijue kwanini alichelewa jana. Hata hivyo sikutaka kumgusa. Nilimuona pale kama Baba Renata, alikuwa kama mtu mgeni kabisa kwangu. Hisia zangu kwake zilikuwa zimekufa kutokana na makosa yake mwenyewe. Sikutaka nimguse kabisa. Ukweli ni kuwa hata yeye mwenyewe sijamruhusu kunigusa kwa namna hiyo kwa karibu miezi saba sasa. Sitaki aniguse kwa sababu makosa aliyoyatenda kwangu bado sijaweza kumsamehe na sikuwa tayari kumsamehe wakati huo. *Wanaume bwana* nilijiambia. Niliamka taratibu nikiwa katika gagulo langu la usiku na kuelekea bafuni ambako kuoga na kujiandaa kwa siku mpya.

Nina kawaida ya kuamka mapema ili kuweza kuandaa mambo mbalimbali ili mzee anapoamka akute breakfast tayari na nguo zake za kwenda ofisini nimemuandalia. Pamoja na mgogoro tuliokuwa nao yeye bado alikuwa ni mume wangu na niliendelea kumpa heshima yake na kufanya mambo yale mengine ambayo yalikuwa yanaendelea kumjengea heshima kwa wafanyakazi hapo nyumbani na hata tunapokwenda nje. Sikutaka kwa namna yoyote ile watu wahisi kinachoendelea kati yangu na yeye na hivyo niliendelea kufanya mambo yale yote mke anatakiwa kuyafanya. Hakuna mtu aliyejua kuwa kule chumbani mgomo umedumu kwa miezi saba sasa. Nakumbuka mara moja hivi kidogo nilimuonea huruma na kumruhusu achukue kwani alikuwa kama na ukame hivi.

Baada ya kuandaa nguo zake pamoja na kuweka kifungua kinywa mezani niliingia kwenye ofisi ndogo ya hapo nyumbani ili kuangalia mipango na ratiba ya siku hiyo ya Jumanne. Nilipekua pekua makaratasi mbalimbali na hasa nilitaka niweze kumshirikisha mzee kuhusu vibali ambavyo nilivipata jana kule Ardhi kuhusu viwanja vya Kunduchi. Asubuhi huwa inanichangamsha sana na leo nilikuwa nimechangamka vya kutosha tu.

Nilikuwa nimezema kwenye kazi hizo niliposikia mlango umefunguliwa na mume wangu alikuwa anabisha kuingia akiuliza kama nilikuwa bize. Nilitabasamu kidogo na kumwambia sikuwa bize namna hiyo. Ukweli ni kwamba pamoja na madudu yake Waziri alikuwa ni mkarimu na mchangamfu. Alikuwa anajua kunipa tabasamu na kunifanya nicheke mara kwa mara. Alisogea karibu yangu.

“Sorry dear, nilichelewa kurudi jana unajua mambo ya sherehe za Muungano yalinitinga” alisema na kunisogelea na

kusimama pembeni yangu. Kabla sijajibu alinirushia busu kwenye shavu langu la kushoto. Nilijihisi kusisimka kidogo na kwa sekunde nikasahau mgomo. Ilikuwa ni sekunde tu! Mgomo ukarudi kwa nguvu zote.
“Ndiyo ukashindwa hata kupiga simu” niliuliza kama kwa hasira iliyochanganyika na wivu kwa mbali.
“I know hun, ningekupigia lakini muda ambao nilipata nafasi ilikuwa tayari very late nikaona nisikusumbue” alisema. Alijaribu kunisogelea kunipa busu kwenye mdomo wangu, nilimtolea nje kwa kugeuza shavu langu jingine.
“Mpenzi ninakumiss sana” alisema kwa sauti yake ya kubembeleza. Najua alimaanisha nini kusema ananimiss.
“Usianze” nilimjibu kwa mkato huku nikianza kujishughulisha tena. Alikaa kimya akijiinua taratibu kuelekea mlangoni. Aliniangalia machoni huku akitikisa kichwa chake kuondoka. Nilijisikia uchungu na nilijisikia hatia; lakini niliamua kuendeleza mgomo hadi atakapokuwa tayari kukubaliana na masharti yangu ambayo hadi wakati huo hakuna dalili ya yeye kuyakubali.

Aliendelea na shughuli zake asubuhi hiyo wakati mimi nilianza taratibu za kuangalia mifugo na shughuli mbalimbali za hapo nyumbani. Kwenye majira ya saa tano hivi mume wangu naye alianza safari zake za kwenda katikati ya jiji baada ya kupitia vibali na kukubaliana na mapendekezo yangu ya nini tuanze kufanya kuhusu viwanja vya Kunduchi. Linapokuja suala la mambo haya ya biashara na uwekezaji mume wangu aliamini sana busara yangu na mara chache alinipinga au kunisahihisha. Aliidhinisha kiasi cha kutumia kwenye mipango ya awali akiniagiza niwasiliane na jamaa wa Morogoro ambao walitujengea ile hoteli yetu ya pale Morogoro ili kuona kama wangeweza kufanya sehemu ya kazi kule Kunduchi.

Baada ya kuondoka niliendelea na shughuli zangu mbalimbali nikiwasimamia wafanyakazi mbalimbali wa ndani na wa kwenye mifugo na shamba. Nilikuwa *nimemsahau* Mjamaika. Nilijishawishi kuwa nimemsahau.

Baada ya chakula cha mchana niliamua kwenda kupumzika kidogo juu na kuacha jua kali la Dar lipite kidogo. Kwa kawaida mida hiyo napenda utulivu ndani ya nyumba na watumishi karibu wote huwa wanaenda kwenye shughuli zao binafsi hadi baadaye jioni kidogo. Ukiondoa msaidizi wa ndani na mlinzi muda huo kunakuwa na ukimya wa kutosha tu.

Nilijilaza kitandani nikiutafuta usingizi. Sikuupata. Mjamaika akanirudia, tena kama kwa kisasi kama katumwa. Nilimuona macho yake ya rangi ya kahawia yalivyolengwa na machozi pale nilipomtishia kumuitia mwizi; niliona akiuma mdomo wake akijizuia kunijibisha; nilimuona vile vile yule mtu aliyemnong’oneza jambo na kumfanya aingie ndani ya kibanda chake. Sijui alimnong’oneza nini. Labda alimng’oneza kuwa mimi ni mke wa waziri. Nilijisikia kinyaa.

Nilijisikia vibaya jinsi ambavyo nilimdhalilisha kijana yule na zaidi nilijisikia vibaya kumvunjia heshima yake mbele za rafiki zake na wanunuzi wengine palena nilifanya hivyo nikijua kabisa hakuwa na jambo lolote ambalo angeweza kunifanya au kulifanya dhidi yangu. Nilikuwa mke wa waziri *ati*. Lakini nilijisikia vibaya kwa sababu sikulelewa hivyo.

Niliona aibu kama mama yangu angeniona nilivyomshushua na kumuadhiri kijana wa watu. Mama yangu asingenitambua kwani tangu utoto tulifundishwa heshima na kuwajali watu. Nilitambua wakati ule kuwa mgongano ule ulikuwa ni ajali kama nyingine na sikutakwa kufanya jambo kubwa namna ile. Nilijiuliza kama yule kijana ana mke au watoto na kama wangeona mume au baba yao anaumbuliwa vile wangejisikiaje. Nilianza kuhisi donge likinikaba kooni. Nilitamani nimkimbilie na kumuomba radhi. Nilitamani nianguke na kusema nimepitiwa tu. Kwa kweli sikujua kwanini najisikia vile kwa mtu wa *chini* kama yeye.

Nilitamani angekuwa karibu nimshike mkono nimsihi anisamehe kwani nilikuwa nimekengeuka tu. Nilitamani anishike mkono na kunituliza, anihakikishie kuwa amenisamehe. Nilitamani anikumbatie na kuniambia *how much he cared for me*, na tena anibusu kwenye midomo yangu, nisikie sauti yake yenye lafudhi ya kijamaika. Nilitamani kijana yule awe mbele yangu nimshike kifua chake na nichezee misokoto ya nywele zake za kirasta. Nimuambie jinsi gani amenigusa moyo wangu. Nilitamani niwe na mjamaika! Nikiwa nimejilaza hivyo, niliukuta mwili wangu wote umewaka kwa tama.

Mawazo yangu hayo yaliamsha hisia zilizokuwa zimelala kwa karibu miezi saba sasa. Nilijisia nahema taratibu na kuta zangu zangu zikiachilia mafuriko taratibu na kunijulisha kuwa nimesisimka kimapenzi. Niliwaka tamaa ya kutaka kujuana na mjamaika kwa namna ya Kibiblia. Moyo ulinidunda na jasho jembamba kwenye paji la uso wangu lilijitokeza kama umande kwenye jani bichi asubuhi. Nilijihisi kutetemeka na kujiuliza ni pepo gani hilo nimeniingia. Nilishindwa kujizuia kuwaza. Nilikuwa ni kama nimewekwa kwenye gari lililoondolewa breki zote na kuachiwa kwenye mteremko.

Nilijikuta naingiza mkono wangu kwenye chupi yangu. Vidole vyangu vyangu viliponisalimu nilishtuka na kubana miguu yangu. Nilishindwa kujizuia kwani mawazo yangu na mjamaika wangu yalienda mbali zaidi. Sikuwahi kufanya hivyo kwa miezi mingi sana kwani sikuwa na sababu lakini nikajikuta najiambia “raha jipe mwenyewe”. Gari lilikosa breki.

Nilimuona akinivuta karibu yake na kunibusu, mikono yake kaizungusha kiunoni kwangu, nilisikia joto la mwili wake na nilisikia akiniambia maneno ya mapenzi, sikujua nimeingiwa na kitu gani mimi. Nilitamani nimuombe msamaha kwa lugha zote nilizojua, nimuambie jinsi gani nimejisikia vibaya. Nimkumbatie, nimbusu, nimpapase na nimfanye vile vyote ambavyo mwanamke kama mimi ningeweza kumfanyia.

Gari lilizidi kuelekea mteremkoni.

Nilizidi kuhema kitandani hapo, macho yangu nimeyafumba na raha ikinizidia. Nilihisi vidole vyake vikikumbatia matiti yangu ambayo chuchu zake zilikuwa zimesimama kwa tamaa. Ulimi wake niliuhisi ukizifyonza chuchu hizo taratibu. Nilisikia raha, raha ilinizidia. Niliuma mdomo wangu wa chini nusura nijitoe damu. Nilitamani kwa kweli angekuwa hapo, nilitamani ndiye yeye angekuwa ananichezea kila sehemu ya mwili wangu. Sijui ingekuwaje, sijuie anatumia manukato gani, sijui, sijui!

Nilitaka kuachia katikati kwani nilizidiwa; nilikuwa hoi kwa tamaa. Yaani, yule kijana ambaye hata sikumjua wala hakunijua namna hiyo ameniingia moyoni hata nashindwa kuelezea. Picha za mapenzi naye zilizidi kichwani mwangu, niko na Mjamaika wangu akinipa raha, raha isiyo na karaha.

Nilijikuta nafika kunako kama mlipuko wa volcano ndani ya tumbo langu. Nilisikia kizazi kitetemeka ndani yangu. Nilibana mkono wangu ndani ya miguu yangu na kujinyosha utadhani niliyeshikwa na kifafa. Nilisikia umeme war aha ukipita kwenye mishipa na mifupa yangu. Niliogopa. Niliogopa kurudia tena kwani sijui ingekuwaje. Nilisikia raha iliyotokana na wazo lililonijia.

Usingizi ulianza kunipitia taratibu mchana huo, huku mwili wangu umelowa jasho. Sikutaka kuamka, sikutaka kufanya nini. Nilitaka nijisikilizie tu. Nilianza kupotea taratibu usingizini. Lakini nilipotea taratibu huku nikiwa nimekusudia jambo ambalo hata sikuwa nimelifikiria kabla yake. Nilijua sikuwa na ujanja isipokuwa hatimaye nifanye kile ambacho moyo ulijisikia tangu nimtie machoni yule mjamaika *wangu.* Nimerudia “wangu” mara ya tatu! Sijui kitu gani kimeniingia mwenzenu. Lazima nijue.
Nitamfatuta nimuombe msamaha. Lazima nimuombe msamaha. Kwa mbali wimbo wa Whitney Houston akiwa na Iglesia “Could I have this Kiss Forever” ulinibembeleza.

Over and over I look in your eyes
you are all I desire
you have captured me
I want to hold you
I want to be close to you
I never want to let go
I wish that this night would never end
I need to know

Could I hold you for for a lifetime
Could I look into your eyes
Could I have this night to share this night together
Could I hold you close beside me
Could I hold you for all time
Could I could I have this kiss forever
Could I could I have this kiss forever, forever

Over and over I've dreamed of this night
Now you're here by my side
You are next to me
I want to hold you and touch you taste you
And make you want no one but me
I wish that this kiss could never end
oh baby please

Could I hold you for a lifetime
Could I look into your eyes
Could I have this night to share this night together
Could I hold you close beside me
Could I hold you for all time
Could I could I have this kiss forever
Could I could I have this kiss forever, forever

I don't want any night to go by
Without you by my side

I just want all my days
Spent being next to you
Lived for just loving you
And baby, oh by the way

Could I hold you for a lifetime
Could I look into your eyes
Could I have this night to share this night together
Could I hold you close beside me
Could I hold you for all time
Could I have this kiss forever
Could I could I have this kiss forever, forever

***